

## SHADDA<sup>1</sup> KATIKA KISWAHILI

Mwansoko, H.J.M.  
Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

### 1.0 Utangulizi

Ingawa shadda ni kipengele muhimu sana katika matamshi ya lugha ya Kiswahili, inaelekea bado hakijapatiwa uzito na ufafanuzi wa kutosha na wanafonetiki wengi wa Kiswahili. Mengi ya marejeo tuliyoypitia yameonyesha kuwa idadi kubwa ya wataalam hawa wamekuwa wakitoa "vidokezo" tu kuhusu mada hii. (Angalia kwa mfano Polome (1967:50-51), Maganga (1979:33), Rubanza (1981)). Baadhi ya makala zilizoshughulikia mahsusi suala la shadda ni makala ya Vitale (1985) na kichocheo cha mjadala kilichotolewa na Temu (1981).

Uchambuzi wa mada hii umeonyesha ufafanuzi mbalimbali za shadda. Kufuatana na maoni ya Temu (1981:1) "neni mkazo (stress) linachukuliwa kwa maana pana ya nguvu litiliwalo tamko fulani likasikika zaidi." Ufafanuzi huu umefanana na ufafanuzi wa shadda wa wanafonetiki wengi wa skuli ya fonolojia ya Ulaya magharibi (k.m. Gleason (1955), Hockett (1958), Hall (1964), ambao kwao shadda ni mchomozo wa sauti ya silabi mojawapo ya neno kutokana na sifa maalum za kifonetiki zinazojitokeza katika silabi hii (taz. 2.0. chini).

Skuli ya fonolojia ya Kirusi (taz. Sherba (1912, 1963), Zinder (1979), Matusevich (1976) ina mtazamo mpana zaidi wa shadda. Kwa maoni ya skuli hii shadda ni ile hali ya mchomozo wa sauti katika silabi mojawapo ya neno (au neno moja katika kifungu kidogo cha maneno, sintagma, au sintagma moja katika fungu kubwa la maneno) kutokana na sifa maalum za kifonetiki zinazojitokeza katika silabi hii tu.<sup>2</sup>

Makala hii italiangalia na kulichanganua suala la shadda kwa kufuata misingi ya skuli ya fonolojia ya Ulaya Magharibi ambayo wanafonetiki wengi wa Kiswahili wanaifuata.

Aidha makala itajaribu kulidadi tena suala la shadda kuwa na sifa za fonimu katika Kiswahili aula, suala ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi wa mwisho.

Hivyo nia ya makala hii ni kuvijadili kwa mapana zaidi vipengele mbalimbali vinavyohusiana na mada ya shadda na kujaliza mapengo yaliyoachwa wazi na wanafonetiki wa Kiswahili waliokwishaongelea mada hii kabla yangu.

### 2.0 Sifa zinazoambatana na shadda

Kwa kawaida shadda huambatana na sifa zifuatazo: kidato, unguvunguvu, muda na ubora wa matamshi.



## 2.1 Kidato

Kidato ni upandishaji na ushushaji wa mawimbi ya sauti wakati wa matamshi. Kwa kawaida kwenye silabi yenye shadda hutokea upandishaji wa sauti. Kwa mfano katika neno "watoto" tunasikia upandishaji wa sauti kwenye silabi [to:] ya katikati ambayo ndiyo iliyo na shadda.

## 2.3 Muda

Imethibitishwa kuwa kila silabi yenye shadda hutamkwa kwa kutumia muda mrefu zaidi ikilinganishwa na silabi zisizo na mkazo. Vyombo maalum vya fonetiki-akustiki vinavyopima muda huu kwa milisekunde vimeonyesha kuwa silabi yenye shadda ni ndefu mara mbili ya silabi isiyo na shadda.

## 2.4 Uboru (wa matamshi ya irabu)

Imedhihirika kwamba vokali iliyo na shadda hujitambulisha kwa uwazi zaidi kuliko ile isiyo na shadda. Kwa mfano katika neno: **marahaba** [maraha:ba] vokali [a:] ya silabi - `ha' - inasikika waziwazi kabisa kuwa ni [a] kuliko vokali a nyingine. Pengine hizi a nyingine zinaweza hata zisisikike vema au zikasikika kwa ufupi sana wakati wa matamshi ya haraka. Mfano [marhá:ba] au hata [márhá:ba].

## 3.0 Kujitokeza kwa shadda:

3.1. Katika lugha ya Kiswahili kila neno (likiwa limesimama pekee na liwapo si kikanusho cha nafsi ya tatu, wakati ujao) huwa na shadda yake ambayo, kwa kawaida, hubainika katika silabi ya pili kutoka silabi tamati (silabi ya mwisho katika neno). Kwa mfano, **múnyu**, **kung'atúka**, **beberú** n.k.

3.2. Lakini hata hivyo kuna baadhi ya maneno, mengi yao yakiwa na asili ya Kiarabu (na Kiajemi) ambayo yanakiuka kanuni hii na badala yake yanakuwa na shadda kwenye silabi ya tatu kutoka mwisho. Kwa mfano:

dhúluma  
thúmni  
gháfula  
áhera

hëshima  
núsura  
lázima n.k.

Namna hii ya uwekaji wa shadda yaelekea kuwa imepokelewa vema katika Kiswahili na haiteli mkwaruzo wowote inaposikika -asikioni. Lakini idadi kubwa ya Waswahili wanaotamka namna hii ni wale walioathiriwa zaidi na lugha ya Kiarabu (yaani Waislamu na wakazi wa pwani). Na kwa kuwa maneno haya yana asili ya Kiarabu, basi matamshi yake ni sahihi kabisa iwapo lengo ni kutamka Kiarabu. Ukiukaji wa taratibu za Kiswahili unajitokeza tu wakati matamshi hayo yanapochukuliwa (na Waswahili walioathiriwa na Kiarabu) kuwa ndiyo ya kisanifu.

3.3. Zaidi ya hapo kuna baadhi ya maneno ambayo yanawekewa shadda ama katika silabi ya pili kutoka mwisho ama katika silabi ya tatu kutoka mwisho na tofauti hizi za nafasi ya shadda hazileti migongano katika kuyaelewa mawasiliano.

Mifano: - tafadháli au tafadhali  
heshima au heshima



lazima	au	lazima
hotuba	au	hotuba
Afrika	au	Afrika
injini	au	injini
ahadi	au	ahadi
kujitahidi	au	kujitahidi n.k.

Kwa kuwa tafauti hizi za uwekaji wa shadda hazibadilishi maana za maneno na kwa hali hii, hazikwamishi mawasiliano zote mbili zimekuwa zikitumika katika Kiswahili sanifu. Lakini tukifuata utaratibu wa kutumia maneno mbalimbali kwa kulingana na mitindo ya mazungumzo tunaweza kuona kwamba uwekaji wa shadda katika silabi ya pili kutoka mwisho (kwa mfano: **tafadhali, heshima...** n.k.) ni sahihi zaidi na ndio unaotumiwa na Waswahili wengi. Matamshi aina ya: **tafadhali, heshima...** n.k. kimsingi hayakubaliani na taratibu za kawaida za uwekaji shadda katika Kiswahili sanifu na kwa hali hii kimtindo hayawezi kukubaliwa kuwa ni sahihi.

**3.4.** Pamoja na hayo yote sio kila ukiukaji wa taratibu za kuweka shadda katika maneno ya Kiswahili yatubidi tu kubali na kuupokea. Uhamishaji wa shadda kutoka silabi ya pili kutoka mwisho hadi silabi ya tatu kutoka silabi tamati katika maneno yafuatayo, kwa mfano, hatudhani kama unaweza kukubaliwa kuwa ni sahihi: **badala, hukumu, fidia** n.k. (Maneno haya yamedondolewa kutoka Redio Tanzania, Dar es Salaam, na hakuna badiliko la maana). Kwa asili yake maneno haya yana shadda inayowiana na taratibu za Kiswahili - yaani katika silabi ya pili toka mwisho. Inavyoelekea shadda hii mpya ni matokeo ya athari ya lugha ya Kiarabu.

#### 4.0 Dhima ya Shadda

Shadda katika Kiswahili ina dhima muhimu mbili.

#### 4.1 Dhima ya kutofautisha homografi

Homografi ni maneno (kwa kawaida mawili) tofauti yanayoandikwa namna moja lakini yanatamkwa namna mbalimbali. Kwa mfano:-

barabara	-	sawasawa
barabara	-	njia ya magari
wataka kazi	-	wewe unahitaji kazi
watakakazi	-	watu wanaotafuta kazi
waenda kasi	-	wewe unakwenda kazi
waenda kasi	-	watu wanaokwenda kasi <sup>3</sup>

#### 4.2 Dhima ya kuyatambulisha waziwazi maneno na maana zake

Neno "ugali," kwa mfano, tunalitambua na kuelewa maana yake kwa sababu limetamkwa kwa kuwekewa shadda yake sahihi. Mabadiliko ya nafasi maalum ya shadda yanaweza kukwamisha utambuzi wa neno hilo na maana yake. Mfano "ugali" na "ugali" (yaelekea kuwa) ni maneno yasiyo na maana yeyote katika Kiswahili.

#### 5.0 Shadda kuwa au kutokuwa na sifa za fonimu katika Kiswahili

Mpaka sasa hakuna msimamo wa pamoja baina ya wanafonetiki wa Kiswahili kuhusu suala hili. Baac<sup>2</sup> i yao (kwa mfano, Polome 1967:51) wanafikiri kwamba shadda inazo sifa za



fonimu. Na ili kuthibitisha hoja hii wanafonetiki hawa wamekuwa wakitoa mfano wa jozi ya maneno:-

barabara (sawasawa) na  
barabára (njia ya magari).

Japo ni kweli kwamba tofautikatika maana za maneno haya mawili zimeletwa na shadda wataalam hawa hawakueleza asili ya maneno haya na wala hawakutoa ufafanuzi wa "**fonimu ni nini**." Kama alivyosema Vitale (1985:107) maneno haya yameingia katika Kiswahili kwa kuazimwa: barábara - yaelekea kutoka Uajemi, na barabára - kutoka Uarabuni. Si maneno ya kiasili na ufonimu wa shadda ya Kiswahili ungefaa uthibitishwe na maneno ambayo yana asili kabisa ya Kiswahili.

Wanafonetiki wengine (mfano Delany, 1967) wanadhani kuwa shadda ya Kiswahili haina ufonimu.

Ingawa Vitale (1985) ameikosoa misimamo ya wataalam wenzake (Delany, Polome) kuhusu ufonimu wa shadda, lakini yeye mwenyewe hakutoa (waziwazi) usuluhisho wa mgongano huu na, kwa hali hii, msimamo wake haujulikani.

Kwa maoni yetu, kabla ya kuamua kama shadda katika Kiswahili ina sifa za fonimu au la, kuna haja kubwa ya kueleza **fonimu ni nini**. Nadharia na ufafanuzi wa fonimu ni wa aina nyingi. Katika makala hii tutatumia ufafanuzi wa mwanafonetiki mhenga wa Kirusi Sherba (1912,1963) anayesema kwamba fonimu ni kishemu cha sauti kilicho kidogo zaidi (hakiwezi kugawanyika tena) katika lugha kinachotofautisha maana na maumbile ya maneno. Mara nyingi maneno haya huwekwa katika jozi wakati yanapolinganishwa, ingawa hii si lazima. Kwa mfano, tofauti (ya maana na maumbile) kati ya maneno "**dogo**" na "**gogo**" zinatokana na fonimu <d> na <g>.

Lakini katika jozi ya maneno "**barábara**" na "**barabára**" kwanza, hakuna fonimu yoyote "**maalumu**" inayoyatofautisha na pili, tofautizake zikokatika maana tu. Maumbile ya maneno haya yanabaki yaleyale (tukichukulia kwamba alama za shadda huwa hazionyeshwi katika maadhishi). Na sifa ya fonimu sio tu kutofautisha maana, bali hata maumbile ya maneno pia, kama ilivyo kwenye mfano wa maneno: "<d> ogo" na "<g> ogo."

Kwa hali hii yaelekea bayana kwamba shadda katika Kiswahili haina sifa za fonimu.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii haikutegemewa kutoa kauli ya mwisho juu ya shadda katika Kiswahili. Tulichokusudia ni kuchochea mjadala baina ya wanafonetiki wa Kiswahili kwa lengo la kutuwezesha kufikia mahitimisho thabiti zaidi kuhusu mtazamo wa shadda katika Kiswahili.

### Tanibihii

1. Istilahi "shadda" kwa maana ya 'stress' imetolewa kutoka kwenye mapendekezo ya **Istilahi za msingi kwa kamusi** yaliyotayarishwa na wanajopo wa TUKI: Prof. Ohly, R., Ndugu Gibbe, A.G., na Ndugu Mkelle, B., Agosti 1978.
2. Kwa kufuata msingi huu wa ufafanuziwa shadda wanafonetiki wa Kirusi hutofautisha aina nne (4) za shadda:

Shadda ya neno (word stress)

Shadda ya fungu la maneno (syntagmatic stress)



Shadda ya msisitizo (logical stress)  
Shadda ya hisia (emphatic/emotional stress)  
(Tafsiri za Kiswahili ni zangu).

3. Mifano hii imedondolewa kutoka kwa Maganga, C. uk. 33.

## Marejeo

- Ashton, E.O., 1944 **Swahili Grammar (Including Intonation)** Longmans, Green and Co. Ltd., London.
- DeLany, M.G.P. 1967 "A Phonological Contrastive Analysis: North-American English-Standard Swahili," **Swahili** 37:27-46.
- Gibbe, A.G., 1977 **Homonymy, Synonymy and Antonymy in Kiswahili:** A lexical study. Tasnifu ya M.A. (Isimu), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Gleason, H.A., 1955 **An Introduction to Descriptive Linguistics.** Holt, Rinehart and Winston, Inc. New York.
- Hall, A.R., 1964 **Introductory Linguistics.** Chilton Books, a Division of Chilton Company, New York.
- Harris, Z.S., 1951 **Structural Linguistics.** University of Chicago Press, Chicago, U.S.A.
- Hockett, C.F., 1958 **A Course in Modern Linguistics.** The Macmillian Company, New York.
- Ladefoged, P., 1975 **A Course in Phonetics.** Harcourt Brace Jovanovich, Inc.
- Loogman, A., 1965 **Swahili Grammar and Syntax.** Duquesne University Press, Pittsburg.
- Maganga, C. 1979 **Misingi ya Fonetiki-Matamshi.** Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha D'Salaam.
- Matusevich, M.I. 1976 **Sarvemenii Ruskii Yaziki. Fonetika.** Maskva "Prosvisheniye" (katika Kirusi)
- Polome', E.C., 1967 **Swahili Language Handbook.** Center for Applied Linguistics.
- Rubanza, Y.I. 1982. "Lafudhi ya Kiswahili: Vidokezo Muhimu. "Makala ya Semina, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu, 20 Novemba, 1981.
- Sherb., L.V. 1912 **Ruskie glasnie V kachestivenam i kalichestvenam atnashenii.** Maskva (katika Kirusi).
- Sherba, L.V., 1963 **Fonetika fransuskava yazika.** Maskva. (katika Kirusi).



Temu, C.W., 1981 "Mkazo katika Kiswahili Sanifu (maswali mawili)." Makala ya Semina ya Fasihi na Isimu, 27/10/1981 - 31/10/1981, Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, Zanzibar.

Tucker, A.N., & Ashton, E.O., 1942. "Swahili Phonetics" katika: **African studies**, vol. 1. No. 2.

Vitale, J.A. 1985. "Aspects of Swahili Stress," **Kiswahili Juzuu** 52/1 & 52/2: 106-113.

Zinder, L.R., 1979. **Obshaya Fonetika**. Maskva "Vwishaya Shkola." (katika Kirusi).